**HOTUBA YA MHESHIMIWA WAZIRI WAZIRI KINDAMBA MKUU WA MKOA WA TANGA KWENYE KUFUNGA MAONESHO YA 10 YA BIASHARA NA UTALII TANGA TAREHE 06 JUNI, 2023.**

**Mhe. Rajab Abdallah Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga,**

**Ndg. Pili Mnyema, Katibu Tawala Mkoa wa Tanga,**

**Ndg. Rashid Mwanyoka, Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara Mkoa wa Tanga,**

**Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Tanga,**

**Mhe. Abdulrahman Shiloow, Mstahiki Meya wa Jiji la Tanga,**

**Wajumbe wa Kamati ya Usalama Mkoa wa Tanga,**

**Wajumbe wa Kamati ya Usalama Wilaya ya Tanga,**

**Viongozi wa Dini,**

**Viongozi wa TCCIA Mkoa wa Tanga,**

**Wakuu wa Taasisi za Umma za Mkoa wa Tanga,**

**Wataalam wa Sekretatieti ya Mkoa wa Tanga,**

**Makatibu Tawala Wilaya za Mkoa wa Tanga ,**

**Wakurugenzi wa Halmashauri za Mkoa wa Tanga,**

**Wafanyabiashara wa Mkoa Tanga,**

**Kamati ya Maandalizi ya Maonesho ya Biashara ya kumi ya Mkoa wa Tanga,**

**Ndugu wanahabari,**

**Mabibi na mabwana…**

***Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!***

**Ndugu washiriki,**

Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia sote kukutana hapa leo hii tukiwa na afya njema. Napenda pia kuishukuru Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo- TCCIA Tanga kwa kunipa heshima kubwa ya kuwa Mgeni Rasmi katika kuhitimisha shughuli za Maonesho ya kumi ya Biashara na Utalii Tanga, yaliyoanza mnamo tarehe 28 Mei, 2023 na kuhitimishwa leo tarehe 06 June, 2023.

Maonesho haya ni ya kumi tangu kuanzishwa kwake mwaka 2013 na yamefanikiwa kupata washiriki kutoka nchi za India, Syria, Malaysia, Pakistan, Kenya, Uganda pamoja na wenyeji Tanzania. Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa washiriki wote kwa kutuunga mkono na kufanikisha maonesho haya. Ni jambo lisilopingika kwamba utayari wenu wa kushiriki umechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya maonesho haya. Ni imani yetu kwamba, mtakuwa tayari kutuunga mkono na kuinua mkoa wa Tanga siyo tu kwa kushiriki katika maonesho yajayo, bali pia katika kushiriki kuwekeza na kufanya biashara katika mkoa wa Tanga ili kuweza kuuinua zaidi mkoa kiuchumi.

***Ndugu washiriki,***

Nichukue fursa hii pia kuipongeza Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya biashara kwa kupunguza gharama za kufanya biashara nchini, na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha uwekezaji unaendelea kukua na kuchangia kwa kiasi kikubwa zaidi kwenye pato la mwananchi mmoja mmoja, Mkoa na Taifa kwa ujumla.

Hata hivyo, Serikali inatekeleza Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji ***Blue Print*** ikiwa ni pamoja na kuboresha utoaji wa huduma za Umma kwa kupunguza utitiri wa kodi, ushuru na tozo ambapo jumla ya Tozo 232 zimefutwa katika mamlaka, na kupunguza kodi ya ongezeko la thamani kwa baadhi ya biadhaa zilizokuwa kero kwa Wafanyabiashara na Wawekezaji.

***Ndugu Washiriki;***

Serikali imejipanga vizuri katika kuwatambua, kuwawezesha na kuwahudumia wawekezaji katika sekta ya viwanda na kuwaondolea changamoto zinazokwamisha uzalishaji wa bidhaa ili waweze kuongeza kasi ya kukuza uchumi wa nchi. Niwaambie tu kwa dhati kuwa, Serikali ya Awamu ya sita inayoongozwa na **Rais makini na Mzalendo namba moja, Mhe. Daktari Samia Suluhu Hassan**, inaendelea kuweka mazingira wezeshi na rafiki kwa wenye viwanda wote na wawekezaji kwa ujumla ili muweze

kufanya shughuli zenu kwa tija na ufanisi, hatimae muweze kutusaidia kuuinua Mkoa wetu wa Tanga.

***Ndugu Washiriki;***

Katika kuhakikisha mazingira ya biashara na uwekezaji yanaboreshwa, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuondoa gharama za viza ili kuwezesha watu watakaotaka kusafiri nchi moja kwenda nyingine kwa shughuli mbalimbali zikiwemo za kibiashara kusafiri kwa urahisi ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi husika. Gharama za viza ni sehemu ya vikwazo kumi (10) visivyo vya kiforodha vilivyoondolewa na Jumuiya inaendelea kushughulikia vikwazo vingine nane (8) vilivyobaki ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara baina ya nchi wanachama.

***Ndugu Washiriki;***

Aidha, Serikali yenu imeendelea kupanua na kuboresha mahusiano na ushirikiano na taasisi binafsi, ikitambua kuwa, sekta binafsi ndio wajenzi, wamiliki na waendelezaji wa Sekta ya viwanda na Biashara nchini. Serikali ya awamu ya sita katika kuendeleza mahusiano mema na sekta binafsi kwenye ujenzi wa uchumi wa nchi yetu itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kwa kutumia sera ya mashirikiano kati ya Serikali na Sekta binafsi *(Public Private Partnership)* ya mwaka 2009. Naomba pia nitumie fursa hii kuwakumbusha kuwa, **hakuna haki bila wajibu**. Wakati Serikali ikiweka mazingira hayo wezeshi, ni wajibu wenu kuiunga mkono kwa kutokuwa wakaidi katika kulipa kodi. Naomba kunukuu maneno ya Mwanahistoria maarufu wa Marekani, Albert Bushnell Hart aliyesema, ***'Taxation is the price which civilized communities pay for the opportunity of remaining civilized'***

akimaanisha 'Ulipaji kodi ni gharama wailipayo jamii iliyostaarabika kwa ajili ya fursa ya kuendelea kuishi kistaarabu'

*Ndugu washiriki*

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naomba niwashukuru wafadhili waliojitoa kuhakikisha maonesho haya yanafana. Mwaka huu, mfadhili mkuu wa maonesho haya ni Mamlaka ya Bandari Tanzania- TPA ambao mbali na kuwa wafadhili, wamekuwa washiriki wa kudumu wa maonesho haya kila mwaka. Wafadhili wengine ni Mamlaka ya Mawasiliano-TCRA, TANGA UWASA, PEE PEE TANZANIA LTD, NMB BANK PLC, Wakala wa Wanyamapori Tanzania-TAWA, GF TRUCK AND EQUIPMENTS bila kuwasahau RADIO MAARIFA, TK FM na RADIO SAUTI YA INJILI kwa kufanikisha matangazo ya radio. Aidha, naomba kwa dhati ya moyowangu niwashukuru Halmashauri Jiji la Tanga kupitia kwa Mstahiki Meya wa Jiji kwa kuridhia maonesho kufanyika katika uwanja huu. Wote kwa pamoja mmewezesha kwa kiasi kikubwa mafanikio ya maonesho haya.

*Ndugu Washiriki;*

Naomba nimalizie hotuba yangu kwa kuwakumbusha na kuwasisitiza washiriki wote wa maonesho haya ya 10 ya Biashara na Utalii na Wananchi wenzangu wa Mkoa wa Tanga kuendela kuchapa kazi kwa bidii na maarifa bila kuvunja Sheria za nchi.

**Baada ya kusema haya, nitamke kuwa Maonesho ya Kumi (10) ya Biashara na Utalii Mkoa wa Tanga yamefungwa rasmi…Ahsanteni kwa Kunisikiliza!**